

UHURU UK 3.

# Dk. Mwinyi aendesha kampeni maskani za wavuvi, mamalishe

**HANIFA RAMADHANI NA EMMANUEL,** ZANZIBAR

MGOMBEA Urais wa Zanzibar kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, jana, aliendelea kuendesha kampeni zake kwa staili ya kuwafuata wananchi wa chini ili kuwasikiliza changamoto zinazowakabili.

Katika ziara yake hiyo, Dk. Mwinyi, alitembelea maskani za wavuvi, mamalishe, waendesha bodaboda na wakulima wa mwani, katika maeneo ya Kijiji cha Kizimkazi, Dimbani, Mkunguni, Makunduchi, Jambiani na Paje.

Akizungumza na wakazi wa vijiji hivyo, Dk. Mwinyi, aliahidi kuviwezesha vikundi vya ushirika kwa kuuongezea nguvu mfuko wa uwekezaji ili kinamama waweze kujiwezesha kiuchumi na kwamba, serikali atakayoiunda atahakikisha inatafuta kila njia kufanikisha jambo hilo.

Mbali na hilo, Dk. Mwinyi alisisitiza kuwa amegombea nafasi hiyo kwa dhamira ya kuwatumikia Wazanzibari, siyo vyenginevyo, ikiwamo kusikiliza changamoto za wananchi na kuzifanyia kazi.

Aliwahakikishia wananchi hao kuwa katika uongozi wake, viongozi atakaowapatia madaraka serikalini, iwe sheha, mkuu wa wilaya au mkuu wa mkoa, wakishindwa kutatua changamoto za wananchi hatowaacha.

"Haiwezekani uwe na wawakilishi katika wilaya na mikoa halafu unalazimika kila siku kuwa pale, kwani wao wana kazi gani? Hili sitalivumilia. Lengo langu ni kuona kila mtu anawajibika katika sehemu yake na karna hatowajibika, atachukukuliwa hatua kali," alisisitiza.

Pia, alisema iwapo atapata ridhaa ya kuiongoza Zanzibar, serikali atakayoiongoza itaondoa dhuluma na upendeleo, hususan katika upatikanaji wa ajira serikalini ili kila Mzanzibari mwenye sifa ya kuajiriwa apate haki.

Mbali na hilo, aliwataka vijana wasio na ajira, kujiandaa kwa fursa mbalimbali zitakazozalishwa, na kuwezeshwa ili waweze kuwa na shughuli za kujiingizia kipato kupitia sekta binafsi kwa kuwa ajira za serikali ni chache.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, serikali ya awamu ya nane, itaweka kipaumbele katika sekta ya uvuvi ili iweze kuwanufaisha wananchi kwa kuwa Wazanzibar wengi hawajanufaika na sekta hiyo.

Alisema serikali itahakikisha inaleta meli kubwa ili ziweze kuvua na kuwa na kiwanda cha kuchakata samaki ili kualeta manufaa kwa pato la taifa na ajira kwa vijana.

Shumbana Ali Haji, mkazi wa Kijiji cha Kizimkazi, Dimbani, alisema Dk. Mwinyi ni mgombea wa kwanza wa urais kufika chini kwa wananchi kwa lengo la kusikiliza kero zao kwa staili hiyo.

Alisema hatua hiyo inazidi kuwapa imani kuwa, CCM na mgombea wake wamedhamiria kuwa upande wa wanyonge.

to,
sha





aji Mark

HABARI KITAIFA

NIPASHE UK 7.

# *Serikali yamega ranchi zake, yagawia wakulima, wafugaji*

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

SERIKALI imemega maeneo kutoka katika mashamba na ranchi zake mikoani na kuwapatia wananchi waliovamia maeneo hayo ili waweze kuendeleza shughuli za kilimo, ufugaji na makazi ikiwa ni juhudi za kutatua migogoro ya wananchi na kulinda maeneo yaliyohifadhiwa kwa misitu na wanyamapori.

Kauli hiyo imetolewa na Victor Mwita, kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wakati akiwasilisha mada kwa waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET), yaliyofanyika kwa njia ya mtandao chini ya Ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Mwita, alisema kuwa wizara hiyo, katika Mkoa wa Ruvuma, imemega hekta 1,800 kutoka katika shamba la Hanga Ngadinda na kuvipatia vijiji vya Gumbirona na Ngadinda huku pia ikimega eneo la hekta 2,208 kutoka Ranchi ya Ruvu na hekta 3,139 kutoka kituo cha Karantini cha Kwala na kuvipatia vijiji jirani ambavyo vimevamia maeneo hayo ya serikali.

Alivitaja vijiji vilivyomegewa eneo la Ranchi ya Ruvu kuwa vipo Wilaya ya Bagamoyo ambavyo ni Ruvu Darajani (hekta 200), Kidogozero (hekta200), Kitonga (hekta 480), Magulumatali (hekta200), Vigazwa (hekta8). Katika Wilaya ya Kibaha, vijiji vilivyomegewa eneo Mperamumbina (hekta 600), Kidomole (hekta 40), Fukayosa (hekta 40), Mkenge (hekta 40) na Milo (hekta 400).

Mwita alivitaja vijiji vilivyomegewa ardhi kutoka Kituo cha Karantini Kwala, kuwa ni vya wilaya za Kibaha ambavyo ni Dutumi (hekta 1,600) Madege (hekta 400), Kwala (hekta 400), Mwembengozi (hekta 400) na eneo la Mkuza Chicks (hekta 179.2), huku kwa upande wa Wilaya ya Bagamoyo, Kijiji cha Visegi -Kitongoji cha Kisogo kilipatiwa (hekta 160), lengo ni kuhakikisha rasilimali za misitu na wanyamapori zinalindwa kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Akizungumzia wafugaji, alisema katika kuhakikisha wanapata maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo yao, wizara hiyo imetenga hekta 48,502.2 kutoka kwenye Ranchi za Taifa na kuwapatia wafugaji kwa utaratibu maalumu na muda mfupi.

Alizitaja ranchi zilizotenga maeneo hayo ni pamoja na Kongwa (hekta 13,591.7), Kalambo (hekta 10,000.0), West Kilimanjaro (hekta 2,416.0), Kikulula (hekta 7,381.6), Misenyi (hekta 10,049.2), Mabale (hekta 1,950.0) na Kigoma (hekta 3,113.7).

Kwa upande wake Dk. Stephen Nindi kutoka Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC), alisema kuwa tayari wameshaainisha maeneo mbalimbali ya shughuli zote za rasilimali za ardhi ikiwamo maeneo ya malisho, ufugaji, kilimo na makazi huku vijiji vyote vikitakiwa kutengeneza mipango ya matumizi ya ardhi kupunguza migogoro inayojitokeza kati yao hifadhi za misitu na wanyamapori.

Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema lengo la mafunzo hayo kwa njia mtandao ni kusaidia serikali kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya uhifadhi wa mazingira na wanyamapori nchini, ili serikali iweze kufikia malengo yake ikiwamo kuondokana na tatizo la ujangili.

Scanned with CamScanner

Mafundi wakiendelea na ukarabati wa barabara ya TRA, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuharibika kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo. **PICHA: FRANK MAXMILLIAN/TUDARCo**

NIPASHE UK 8.

# Wafugaji kupeleka maziwa nje ya nchi

**Na Renatha Msungu, ARUSHA**

WAFUGAJI kutoka Kanda ya Kaskazini wamepata kibali cha kupeleka maziwa nje ya nchi, jambo ambalo litawezesha kupata kipato zaidi na kuondokana na ukosefu wa masoko.

Akizungumza na waaandishi wa habari Mkurugenzi Mtendaji wa Kilimanjaro Fresh, Irfhan Virjee, alisema wanatarajia kuanza kupeleka maziwa nchini Kenya kama moja ya upanuzi wa soko la maziwa.

"Tunakaribia kuanza kupeleka maziwa nchini Kenya lengo ni kupanua soko la wafugaji wetu hapa nchini," alisema.

Alisema hivi sasa kiwanda chao kinakusanya maziwa kiasi cha lita 10,000, lakini matarajio yao ni kukusanya lita 72,000 ambazo zitajitosheleza katika usambazaji.

Kwa Mujibu wa Mkurugenzi huyo, wamejipanga kutembelea wafugaji ili kuhakikisha wanapata maziwa ya kutosha katika nchi za jirani kwa ajili ya kukuza soko.

Alisema kupitia bidhaa za Kilimanjaro Fresh wafugaji wengi wamenufaika kutokana na soko lao kuwa pana ambapo hivi sasa wafugaji wataanza kunufaika na soko hilo.

Alisema wamejipanga kuhakikisha soko linakua na wafanyabiashara ya maziwa watanufaika sana kutokana na upanuzi wa soko ndani na nje ya nchi.

Naye Mdhibiti ubora wa Kilimanjaro Fresh, Subira Shabani, alisema maziwa kabla ya kupelekwa sokoni ili kuhakikisha kila yanapokwenda yanakuwa salama kwa walaji.

Subira alisema maziwa yanayosambazwa na Kilimanjaro Fresh yana soko kubwa ndani na nje ya nchi.

"Tumejipanga kuhakikisha bidhaa zinakuwa bora na soko linakuwa kubwa kutokana na umaridadi wa maziwa waliokuwa nayo," alisema Subira.

Naye mfugaji Lukumay John, alisema kabla ya kiwanda cha Kilimanjaro Fresh wafugaji walikuwa wakipata hasara kutokana na maziwa kuharibika.

Alifafanua zaidi ya kuwa hivi sasa maziwa hayawasumbui tena kutokana na kiwanda hicho kukusanya lita 10,000 za maziwa kutoka kwa wafugaji na kwamba wafugaji hivi sasa hawana shida yoyote kuhusiana na soko la maziwa ambayo awali ilikuwa ni changamoto kubwa.

Scanned with CamScanner

za

za ya masuala
ni na Historia.
hadi 1958
isi ya Ustawi
e Hague na
na ya masuala

hadi 1961
o Kikuu cha
Jingereza na
ida ya kwanza
'ati Bomani
ua na kupata
Afrika Kusini
ilikuwa nzuri
a katika kazi
eria, lakini hali
afla na alifariki
10, 2020 na
oto watatu na

ihudhuliwa na
bali akiwemo
Awamu ya Pili,
yi na mkewe
Mstaafu wa
akaya Mrisho
uu Mstaafu,
de Othman,
nian Lubuva,
u Barnabas
asheria Mkuu
rdus Kilangi.



oto

ja na kupata

Mkuu huyo
ifumo huo
wataalam wa
akisi mahitaji
utaimarisha
na nyaraka
za gharama
ulipiaji leseni
wa ikitumia
aka ambazo
ika miradi ya

a niaba ya
hayo, Mkuu
na Utawala,
nanus Kilaja,

MAJIRA UK 7.

# Vifaranga vya kuku vyaadimika Kisutu

**Na Mwandishi Wetu**

WAFUNGAJI wameshtushwa na ongezeko la bei ya vifaranga vya kuku kutoka sh. 1,200 kwa kifaranga kimoja hadi sh. 2,000, hali inayoashiria uwezekano wa kupanda kwa bei ya kitoweo hicho.

Baadhi ya wananchi waliozungumza jana wamesema kutokana na uhaba huo, wanalazimika kununua vifaranga kwa bei ya juu.

Muuza kuku, Ramadhani Ally kutoka soko la Kisutu jijin Dar es Salaam alisema biashara hiyo kwa sasa sio nzuri kulingana na idadi ya kuku waliopo sokoni.

Kwa mujibu wa mfanyabiashara huyo uhaba huo wa vifaranga unatajwa kusababishwa na janga la Corona. "Janga la Corona limechangia kuadimika bidhaa ya kuku sokoni," alisema na kutoa wito kwa wazalishaji wa kuku ikiwemo Interchick kuongeza uzalishaji zaidi ili kwenda sambamba na mahitaji ya sokoni kwa sasa. "Wiki mbili kabla ya sasa kwa siku za mwanzoni tulikuwa tunauza kuku 150 hadi 100 kwa siku, lakini mauzo hayo sasa yamebaki kama historia, kwani mauzo yameshuka hadi kufikia kuku 50 kwa siku," alisema na kuongeza kuwa kuku mmoja sh. 6,500.

Alisema wanunuzi wa kuku wanategemea sana hali ya soko la wauuzaji na idadi mauzo huongezeka kulingana na mahitaji ya siku hiyo, kwani kama soko ni zuri muuzaji anaweza kununua kuku 500 kwa siku na akawauza wote.

Kwa mujibu wa wa mfanyabiashara huyo wateja wa kuku wamepungua ikilinganishwa na siku za nyuma. "Wateja wanakuja mara moja, lakini hawarudi tena baada ya ushuru kupanda kutoka sh. 500 hadi sh.1, 000 kwa siku, hivyo kila mfanyabiashara anayemiliki banda anatakiwa kulipa ushuru sh. 30,000 kila mwezi bila kujali umeuza au hujauza kuku kwa mwezi huo," alisema Anuary Yusuph.

Alitoa angalizo kwa baadhi ya vijana ambao wapo kwenye biashara hiyo kuwa wavumilivu, kwani huenda hali hii ikabadilika na changamoto hiyo ikatoweka kabisa.

Naye Mtunza Hazina wa Soko la Kisutu, Ally Vulu ,alisema idadi ya wauza kuku ambao wanalipa ushuru wa sh. 1,000 ni zaidi 120, hivyo alishauri ushuru huo upunguzwe kwani hali ya biashara kwa sasa ni mbaya. Aliongeza kuwa upungufu kwa wateja na wanunuzi wa kuku ambao kwa kiwango kikubwa ni akina mama lishe, wauza chips na watu mbalmbali.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Soko la Kisutu, Zuberi Luono amedhibitisha kuwepo kwa hali hiyo sokoni hapo na kuziomba mamlaka serikalini hususani Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha uzalishaji vifaranga unaongezeka.

Scanned with CamScanner

**Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Raymond Magwala (kushoto) akimkabidhi ilani ya CCM mgombea Udiwani wa Kata ya Upanga Mashariki, Sultan Salim.** (Picha na Heri SHaaban)

MAJIRA UK 9.

# Ujenzi Soko la Samaki kugharimu bil. 13/-

**Na Judith Ferdinand, Mwanza**

UJENZI wa Soko la Samaki la Kirumba lililopo wilayani Ilemeka Mkoa wa Mwanza, unatarajia kugharimu sh. bilioni 13 ikiwa ni mkakati wa serikali kuwainua wananchi kiuchumi na kuongeza pato la taifa.

Akizungumza na wakazi wa Kata ya Kirumba mgombea Ubunge kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Jimbo la Ilemela, Dkt. Angeline Mabula waliohudhuria mkutano wake wa kampeni kwa ajili ya kuomba kura, uliofanyika Uwanja wa Bujumbura Mtaa wa Kabuhoro alisema endapo akichaguliwa atahakikisha anasimamia ujenzi wa Soko la Kirumba kwa kiwango cha kisasa zaidi kuliko Soko la Kariakoo.

Alisema pia atasimamia miundombinu muhimu ya kuingilia sokoni humo, ikiwemo ujenzi wa barabara zote zinazoingia ndani ya soko kwa kiwango cha lami.

Dkt. Mabula aliwaomba wananchi hao kukiamini chama chake na kumpigia kura nyingi mgombea wa nafasi ya Urais, Dkt. John Magufuli kama shukrani kwa namna alivyosaidia utatuzi wa migogoro ya ardhi ya muda mrefu iliyokuwa kero kwa wananchi hao, ikiwemo mgogoro wa ardhi Kigoto kati ya Jeshi la Polisi na wananchi, ambao umeamuliwa ambapo jeshi hilo kubaki na eneo kidogo wakati eneo lililobaki likichukuliwa na wananchi na kumilikishwa.

Alisema mgogoro mwingine wa ardhi ni wa Lukobe kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na wananchi wa mtaa huo, ambapo uthamini umefanyika na wananchi wameanza kulipwa fidia pamoja na mgogoro wa ardhi Nyagunguru Ilemela ambapo wananchi wameanza kulipwa fidia.

Kwa upande wake Meneja Kampeni wa CCM Jimbo la Ilemela, Kazungu Idebe alikemea upotoshwaji unaofanywa na baadhi ya wagombea kutoka vyama vya upinzani na kutoa lugha zisizofaa wakati wakiomba kura kwa wananchi, huku akisisitiza kuwa suala la uchaguzi ni hiari ya wananchi kukichagua chama gani na mgombea gani, hivyo kuwaomba kufanya siasa safi sanjari na kusisitiza amani na utulivu.

Scanned with CamScanner



ANATOSHA: Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akimnadi mgombea ubunge wa CCM Jimbo la Tanga mjini, Ummy Mwalimu, mwishoni mwa wiki.

KATAVI

MTANZANIA UK 9.

# Mlele yagawa ekta 10,000 za ardhi kwa wafugaji

**Na WALTER MGULUCHUMA**

WILAYA ya Mlele mkoani Katavi, imegawa zaidi ya ekta 10,000 za ardhi kwa ajiri ya kuwagawia wafugaji kwa sababu inataka kuwa na ufugaji wa kisasa zaidi.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera wakati wa ugawaji wa vitalu 10 kwa ajiri ya wafugaji vilivyotolewa na uongozi wa wilaya hiyo, baada ya Serikali kurudisha maeneo ya mistu iliyokuwa inamilikiwa na Wakala wa Mistu Tanzania (TFS) kwa wananchi .

Homera alisema wilaya hiyo imegawa ardhi kwa ajiri ya vitalu vya wafugaji yenye ekta 10,500 kwa ajili ya mifugo, ikiwa ni mkakati wa kuifanya kuwa yakisasa zaidi kwa kuwa hataki kuona yanatokea malalamiko ya wakulima na wafugaji .

Alisema wafugaji wa wilaya hiyo, wamekuwa wakidumisha amani na ndiyo maana hayajawahi kutokea matukio makubwa ya uhalifu kwenye wilaya hiyo na kuifanya iendelee kuwa salama zaidi hivyo kama kuna mtu anataka kuwekeza eneo lipo .

Alisema wamekuwa na tabia moja ya kufuga na kulima ndiyo maana wilaya imeamua kutenga pia maeneo ya wakulima pia kwenye eneo la Kamalampaka na wafugaji wametengewa maeneo ya Kamsisi na Mapili .

Aliwaonya wafugaji wasitumia vibaya maeneo hayo waliyopewa kwa kukata miti ovyo, bali miti waliyoikuta wakate tuu kwenye eneo ambalo mtu anaweza kujenga na si vinginavyo vinginevyo wanaweza wakasababisha jangwa .

Aliwataka wananchi wa mkoa huo watunze maeneo ya ardhi yao na waache kuuza kwa bei ndogo watambue kuwa kuna wawekezaji wanakuja na idadi ya ng'ombe imekuwa ni wengi kuliko binadamu nandio maana wameanzisha utaratibu wa kugawa maeneo hayo ili migogoro isije ikatokea.

Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Rachae Kasanda alisema kuwa kilio cha wananchi wa wilaya hiyo kwa muda mrefu ilikuwa ni ni eneo kubwa, ni Hifadhi ya Taifa ya Katavi na hifadhi za mistu.

Alisema TFS wamatoa eka 24 ,000 ambazo walikuwa wakizimiliki kwa ajiri ya wananchi kama ambavyo Serikali ilivyoagiza baadhi ya maeneo ya mistu yarudishwe kwa wananchi hivyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mlele, Alex Kagunze alisema ekari 2,400, zimetengwa Kijiji cha Mapili kwa ajili ya uanzishwaji wa kiwanda cha nyama na hadi sasa wafugaji 102 wameishaanza kuchangia ujenzi wa kiwanda hicho .

Mfugaji wa mifugo wa kutoka Kijiji cha Kingwamizi, Bubele Suluja aliishukuru Serikali kuwapatia vitalu vya kufugia mifugo yao, kwani walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya kukamatwa mara kwa mara kwa kosa la kuchungia mifugo yao kwenye Hifadhi ya Taifa na kwenye mapori ya akiba .

DODOMA

Scanned with CamScanner



# Lipumba atoa ahadi tatu kwa wafugaji

Fortune Francis,Mwananchi
ffrancis@mwananchi.co.tz

**Dodoma.** Mgombea urais kupitia Chama cha Wananchi ( CUF), Profesa Ibrahim Lipumba ameahidi mambo matatu kwa wakulima na wafugaji wa mkoani wa Dodoma ikiwamo kuwawezesha kupata masoko kwa njia ya mtandao.

Akiwa ameambatana na mgombea mwenza Hamida Abdalah, alitoa ahadi hizo jana wakati akihutubia wananchi wa eneo la Chalinze Nyama wilayani Chamwino.

Alisema mifugo kama mbuzi ni zao la biashara ndani na nje ya nchi, lakini wafugaji hawanufaiki kutokana na kutokuwapo kwa utaratibu unaoweza kuwahakikishia kuwa na ufugaji bora.

"Wenzetu wa Afrika ya Kati wanapenda mbuzi waliopata malisho ya kawaida, kwa hiyo ufugaji wa mbuzi unalipa si tu ndani, hata nje ya nchi," alisema Profesa Lipumba na kuongeza kuwa ili mbuzi waweze kuwa na soko, lazima wafanyabiashara wajue kufanya biashara kupitia mitandao na kujenga utaratibu wa vijana kujielimisha.

"Sera ya CUF ni kuhakikisha inawekeza kwa vijana na kuhakikisha wanapata elimu bora ya biashara kwa njia ya mtandao kuanzia shule za awali, shule za msingi na sekondari," alisema.

Kuhusu ng'ombe, alisema wamekuwa wakifugwa kienyeji badala ya kutumia utaalamu wa kisasa kupata ng'ombe wazuri wenye maziwa ya kutosha.

"Bado hatujatumia mifugo yetu kuhakikisha tunajitegemea vizuri kwa maziwa. Tunahitaji kuboresha ufugaji ili ng'ombe waweze kutoa maziwa ya kutosha kwa ajili ya biashara," alisema.

### Ahadi zake kwenye kilimo

Akizungumzia suala la kilimo, Profesa Lipumba alisema katika ilani ya chama hicho wamedhamiria kuboresha kilimo, ili mkulima wa kawaida alime kilimo cha kisasa na kupata chakula cha kutosha.

Alisema mazao kama mtama, uwele na ulezi, yana soko kubwa duniani, kwa kuwa nchi nyingine hutumia mazao hayo kwa chakula cha wanyama.

"Mazao haya yana soko kubwa ndani na nje ya nchi kama tutaweka utaratibu mzuri, Wachina wanahitaji tani nyingi za mtama kwa ajili ya kulishia mifugo yao," alisema.

Aidha Profesa Lipumba alibainisha kuwa Tanzania inahitaji kuweka utaratibu mzuri wa kufanya mtama kuwa zao la biashara ili wananchi waweze kufaidika na zao hilo.

Profesa Lipumba ambaye pia ni mwenyekiti wa chama hicho alisema ipo haja ya kuweka utaratibu wa kulinda mazingira kulingana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

"CUF tumejipanga kushirikiana na wananchi kuleta mabadiliko katika kuhifadhi mazingira na mambo haya yanawezekana kama mkituchagua. Tunahitaji kuwa na uongozi utakaofuata taratibu katika kushirikisha wananchi," alisema.

Naye mgombea ubunge jimbo la Chamwino, Diana Simba alisema hali katika jimbo hilo ni ngumu kutokana na ubovu wa miundombinu.

Alisema angekuwa mbunge angesimamia vizuri fedha za mfuko wa jimbo, ili kusiwe na matatizo kwenye jimbo hilo.

"Nitakapokuwa mbunge nitatumia vizuri fedha za mfuko wa jimbo kutatua changamoto zinazotukabili. Naomba mnichague ili niweze kukayafanyia kazi haya matatizo.


Diana pia alikana uvumi kuwa kama upinzani utachaguliwa, Ikulu itarejeshwa kuwa jijini Dar es Salaam. Alisema Lipumba akichaguliwa ataendelea kukaa Chamwino anapokaa Rais John Magufuli.

**NUKUU MUHIMU**

**"CUF tumejipanga kushirikiana na wananchi kuleta mabadiliko katika kuhifadhi mazingira na mambo haya yanawezekana kama mkituchagua. Tunahitaji kuwa na uongozi utakaofuata taratibu katika kushirikisha wananchi," alisema Profesa Lipumba.**

**Katika mikutano yake mingine, Lipumba amesema: "Kipindi ambacho Serikali ya CCM imekaa madarakani, imekuwa haitilii mkazo suala la kilimo na kusababisha kuzorota kwa sekta ya viwanda.**

**"Bila kufanya mapinduzi ya kilimo huwezi kuleta mapinduzi ya viwanda, hivyo sera ya CUF ni kuleta mabadiliko katika kilimo."**



Scanned with CamScanner